



HALMASHAURI YA MANISPAA MOROGORO



ZABUNI NA: LGA/079/2022-23/HQ/NCS/01

TAREHE: 15/08/2022

TANGAZO LA ZABUNI YA UPANGISHAJI WA ENEO LA "ROCK GARDEN" KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO

1. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inakusudia kupangisha eneo la "Rock Garden" iliyopo katika makutano ya barabara ya Rwegasore na Boma. Eneo hilo lina ukubwa wa ekari nne (4) na liko umbali wa kilometa tatu (3) kutoka katikati ya Mji. Eneo hilo linafaa kwa kutumika kwa shughuli za kivutio cha Watalii chenye bustani na mazingira ya uoto wa asili, sehemu za mapumziko katika siku za mwisho wa wiki pamoja na shughuli mbalimbali za burudani.
2. Zabuni hii itaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 (2011) na Kanuni zake za mwaka 2013, Tangazo la Serikali Na. 446 na marekebisho yake ya mwaka 2016.
3. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inawakaribisha Makampuni, Vikundi au watu binafsi wenye nia na uwezo wa kupangisha katika eneo la "Rock Garden".
4. Nyaraka za Zabuni zitapatikana baada ya kulipa ada ya Tshs. 100,000/= (Ada hiyo haitarejeshwa) na utaratibu wa malipo unapatikana Ofisi ya Mkukrugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa S.L.P. 166.

Sifa za mwombaji:

- i. Mzabuni awe na uwezo wa kifedha wa kutosha kwa ajili ya kuendesha biashara atakayoifanya kwenye eneo hilo pamoja na kuboresha mazingira ya bustani hiyo.
- ii. Awe na namba ya mlipa kodi (TIN Number)
- iii. Awe na uwezo wa kulipa kodi ya pango itakayokubaliwa na Manispaa kwenye zabuni.
- iv. Muombaji anaruhusiwa kuwasilisha "proposal" (Rasimu) ya uboreshaji wa eneo hilo.

- v. Awe na uzoefu wa kuendesha maeneo ya shughuli za burudani na ataje majina ya maeneo hayo mahali yalipo, kama anayamiliki au amekodishwa na kama amekodishwa aonyeshe mikataba aliyoingia.
5. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani ya muombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi yake ilipo kwa sasa.
 6. **ZINGATIA:** Fomu ya maombi ya zabuni ijazwe na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (power of Attorney) katika zabuni hii.
 7. Muombaji atatakiwa aambatanishe nyaraka mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye kitabu cha zabuni.
 8. Muombaji aambatanishe kivuli cha stakabadhi ya ada ya maombi wakati wa kurejesha zabuni.
 9. Waombaji wanaweza kukagua nyaraka za zabuni na kupata maelezo kutoka kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro S.L.P. 166 Morogoro siku ya Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za Sikukuu za Kitaifa.
 10. Muombaji wa zabuni anahitajika kuleta kiapo cha dhamana (bid securing declaration) kama kilivyoainishwa kwenye kitabu cha zabuni.
 11. Masharti na vigezo vingine vinapatikana katika kitabu cha zabuni.
 12. Zabuni zote ziwe na nakala halisi (original) moja na nakala kivuli mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Zabuni Na. **LGA/079/2022-23/HQ/NCS/01 (ingiza maelezo ya zabuni unayoomba)** Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa anuani ifuatayo:- **Mkurugenzi wa Manispaa, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, S.L.P 166, Morogoro.**
 13. Siku ya mwisho ya kuwasilisha zabuni ni **tarehe 29 August, 2022 saa (4.00) nne kamili asubuhi.** Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu, mbele ya wawakilishi wa wazabuni watakaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni hizo katika ukumbi wa Manispaa.
 13. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielektroniki, na Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji Zabuni, kwa hali yoyote ile Zabuni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.



Ally H. Machelo

**MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO**

**MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO**